JINA……………………………………………………………………………...............NAMBARI………………………….............

SHULE………………………………………………………………………………..................MKONDO…………………….............

# MTIHANI WA PAMOJA WA NYAHOKAKIRA AWAMU YA TATU, 2022

MTIHANI WA MWIGO

***Cheti Cha kuhitimu elimu ya sekondari nchini Kenya***

**Kidato cha nne**

102/1

Kiswahili inshaKaratasi ya 1

Muda: saa 1 dakika 45

**Maagizo**

I). Jibu maswali **mawili** pekee ii).Swali la **kwanza** ni la **lazima**

iii).Chagua insha ya pili kutoka kwa zile zilizosaliaiv).Kila insha isipungue **maneno 400**

v).Insha zote ziandukwe kwa **lugha ya Kiswahili**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama | Sahihi |
|---|---|---|---|
| 1 | 20 | | |
| | 20 | | |
| JUMLA | 40 | | |

1.Visa vya vijana wengi katika ndoa katika eneo la Tamuchungu kujiua au kuuana na wapenzi wao vimeongezeka.Wewe kama mwanahabari umepata fursa ya kumhoji chifu wa eneo hilo kuhusu vyanzo vya visa hivyo na suluhu .Andika mahojiano hayo

2.’’Sekta ya bodaboda ina athari mbaya katika jamii” .Thibitisha

3.Andika kisa kinachoafiki maana ya methali : Subira huvuta heri

4.Andika kisa kitakachomalizia kwa kauli ifuatayo

…na katika uchaguzi wa marudio uliofanywa baada ya kisa hicho,bwana Tendakazi akapata ushindi mkubwa na kuwa mbunge wa eneo la Tandale

**MWONGOZO**

**1.*Visa vya vijana wengi katika ndoa katika eneo la Tamuchungu kujiua au kuuana na wapenzi wao vimeongezeka.Wewe kama mwanahabari umepata fursa ya kumhoji chifu wa eneo hilo kuhusu vyanzo vya visa hivyo na suluhu .Andika mahojiano hayo.***

**1.**Kichwa kiwe na neno mahojiano,wahusika na mada

2. Utangulizi

Huwa ni maelezo mafupi ambayo huwa kwa mabano kujumuisha kiini cha mahojiano, mahali, mhoji na mhojiwa walipo, majina na vyeo vyao, hali zao na wakati pia hudokezwa.

3. Mwili

Huandikwa mtindo wa kitamthilia.

Maneno au maelezo ya mhoji na mhojiwa huandikwa baada ya koloni.

4. Hitimisho

Mhoji anaweza kutoa kauli ya kuonyesha kukamilika kwa mahojiano kwa kumshukuru mhojiwa kwa kuhudhuria kisha baadaye maagano kutolewa kwa mabano kwa mfano (**Wanasalimiana na kuondoka)**

**MAUDHUI**

**Vyanzo/ visababishi**

1.Ukosefu wa ushauri nasaha kabla ya ndoa
2.Ndoa za mapema
3.Matumizi ya dawa za kulevya
4.Kupanda kwa gharama ya Maisha
5.Vijana kutegemea wazazi wao kwa kila kitu wakiwa wakubwa wanashindwa kujitegemea
6.Ukosefu wa uaminifu katika ndoa
7.Ushindani katika ndoa
8.Ukosefu wa heshima katika ndoa
9.Kutamauka
10.Kuiga mifano mibaya kutoka kwa wazazi au wengine kwenye ndoa
11.Utepetevu wa sheria dhidi ya wanaotekeleza visa hivi
12.Athari ya mitandao
13.Kutothamini ndoa
14.Ukosefu wa mafunzo ya dini
15. Umbeya au Habari za uwongo

**Suluhu**

1.Ushauri nasaha kabla na wakiwa kwenye ndoa
2.Wazazi kufunza wanao kujitegemea
3.Vijana wajikimu kabla ya kuingia kwenye ndoa
4.Vijana wafunzwe kuwa wavumilivu
5.Talaka
6.Kufufua mila na tamaduni za kiafrika hasa mviga ya ndoa
7.Mafunzo ya dini kutolewa
8.Kuhamasishwa kuhusu athari ya dawa za kulevya
9. Kuchukua mkondo wa sheria panapotokea mtafaruku kwenye ndoa

**<u>Tanbihi</u>**

- ✓ Mtahiniwa ajihusishe na mahojiano
- ✓ Maudhui yawe sita
- ✓ Ashughulikie pande zote mbili
- ✓ Pande moja asipite 10/20
- ✓ Iwapo mwanafunzi akiwa na maudhui
    - 5 =10/20
    - 4=09/20
    - 3=08/20
    - 2=07/20
    - 1=06/20
    - kutajataja maudhui=05/20
    - Sura ya insha 04/20
    - kupotoka= 03/20

***2.''Sekta ya bodaboda ina athari mbaya katika jamii" .Thibitisha***

**<u>Kuunga mkono(athari mbaya)</u>**

1. Ajali
2. Vifo
3. Msongamano barabarani
4. Wizi wa kimabavu
5. Kusababisha magonjwa kwa mfano ugonjwa wa pumu
6. Vita
7. Wanafunzi kusitisha masomo kujiunga na sekta hii
8. Baadhi yao kuwahadaa wasichana wadogo kuzini nao
9. Uchafuzi wa mazingira
10. Hubeba idadi ndogo ya wasafiri

**<u>Kupinga (athari nzuri)</u>**

1. Kurahisisha usafiri
2. Ujira
3. Rahisi kupenya kwenye msongamano
4. Rahisi kupata maeneo ya kuegesha

5. Ushuru unaotozwa ni wa chini ukilinganishwa na magari
6. Bodaboda hupenya kwenye maeneo ambayo magari hayawezi pita
7. Hutumia kiwango cha chini cha mafuta
8. Wahudumu wa pikipiki kupatikana kwa urahisi wakati wowote

***Tanbihi***

- ✓ Maudhui yawe sita
- ✓ Ashughulikie pande zote mbili
- ✓ Pande moja asipite 10/20
- ✓ Iwapo mwanafunzi akiwa na maudhui
  - 5 =10/20
  - 4=09/20
  - 3=08/20
  - 2=07/20
  - 1=06/20,
  - Kutojataja maudhui=05/20
  - kupotoka= 03/20

***3.Andika kisa kinachoafiki maana ya methali : Subira huvuta heri***

- ✓ Ni insha ya methali
- ✓ Ina pande mbili
- ✓ Andika kisa kinachoafiki maana na matumizi ya methali
- ✓ Kisa kikikosa kulenga matumizi atakuwa amepotoka kimaudhui atuzwe 03/20
- ✓ Maana..uvumilivu katika jambo au hali fulani baadaye huleta afueni
- ✓ Kisa kiwe kimoja

4***.Andika kisa kitakachomalizia kwa kauli ifuatayo***

***…na katika uchaguzi wa marudio uliofanywa baada ya kisa hicho, bwana Tendakazi akapata ushindi mkubwa na kuwa mbunge wa eneo la Tandale***

1.Atunge kisa kinachoonyesha sababu ya marudio ya uchaguzi katika eneo la Tandale
2.Uchaguzi ulirudiwa labda kwa sababu ya mbunge wa awali kuhusika katika wizi,kifo,uamuzi wa korti,mchafuko wa uchaguzi na uchaguzi kusitishwa.

**Tanbihi**

- ✓ Kisa kiwe kimoja na cha kusisimua
- ✓ Awe na kichwa akikosa aadhibiwe kimtindo
- ✓ Kisa kilenge uchaguzi,asipolenga uchaguzi atapotoka kimaudhui na apate 03/20
- ✓ Asipoonyesha sababu za kurudiwa kwa uchaguzi asipite 10